# JARIDA MAALUM

## OFISI YA WAZIRI MKUU
## KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

Toleo No. 2 | DISEMBA, 2020



+255 026 2963450
ps@kazi.go.tz
www.kazi.go.tz
Kazi Street, Mji wa Serikali
Mtumba, DODOMA



# WAZIRI MHAGAMA AANZA KUTEKELEZA AGIZO LA RAIS MAGUFULI

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Jenista Mhagama amewataka watendaji wa wizara yake kuhakikisha wanakamilisha mfumo wa vibali vya kazi kwa raia wa kigeni haraka ili kuondokana na changamoto zilizopo katika utoaji wa vibali hivyo.

Kauli hiyo ameitoa Jijini Dodoma Disemba 12, 2020 wakati alipokutana na Menejimenti ya wizara yake na taasisi zilizopo chini ya ofisi hiyo ambapo alieleza kuwa usimikaji wa mfumo wa kielektroniki wa kushughulikia vibali vya kazi itasaidia kuimarisha ushughulikiaji wa maombi ya vibali vya wageni.

"Idara ya Kazi kwa mujibu wa sheria inajukumu la kuratibu ajira za wageni nchini, hivyo kutokana na changamoto zilizopo katika utoaji wa vibali hivyo hivyo suluhisho pekee la kutoa vibali kwa wakati ni kuharakisha mfumo wa kielektroniki ambao utashughulikia vibali vya kazi," alieleza Waziri Mhagama

Aliongeza kuwa, Mfumo huo wa kielektroniki ambao unaandaliwa utakuwa na manufaa ikiwemo kuongeza ufanisi katika kushughulikia maombi ya vibali vya kazi na kuokoa muda wa kushughulikia maombi ya vibali hivyo.

Wakati akiapisha baraza jipya la Mawaziri Disemba 9, 2020 Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alieleza kuwa bado kuna changamoto upande wa kazi hususan kwenye ushughulikiwaji wa vibali vya kazi na aliwataka mawaziri kushughulikia suala hilo.



Inaendelea Uk. 2

Aidha, Waziri Mhagama alisisitiza suala la uboreshaji wa sheria za kazi ili ziendane na mfumo huo unaoandaliwa.

"Hakikisheni mnafanya mapitio sheria za kazi kwa kushirikisha wadau ambao wanahusika katika uandaaji wa mfumo huo ili kuboresha utoaji wa huduma katika kushughulikia maombi ya vibali," alisema Mhagama

Sambamba na hayo, Mheshimiwa Mhagama ameagiza kuwepo na utaratibu wa kushughulikia malalamiko mbalimbali yanayohusu vibali vya kazi ambayo yanatolewa na wadau.

Waziri Mhagama amekutana na Menejimenti ya ofisi yake pamoja na Taasisi zilizopo chini ya ofisi hiyo lengo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa anafungua Bunge la 12 na pia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha Miaka mitano (2020 – 2025).



Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Ndg. James Kajugusi (aliyesimama) akitoa taarifa fupi wakati wa kikao kazi cha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Jenista Mhagama.

# OFISI YA WAZIRI MKUU IMEJIPANGA KIUTENDAJI: WAZIRI MHAGAMA



**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Jenista Mhagama amesema Ofisi ya Waziri Mkuu imejipanga kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kasi zaidi ili kuendana na kasi ya serikali ya Awamu ya Tano.**

**Kauli hiyo imetolewa na Waziri wenye dhamana ya Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Jenista Mhagama mara baada ya kupokelewa rasmi katika Ofisi ya Waziri Mkuu iliyopo Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma hii leo Disemba 10, 2020.**

**Waziri Mhagama alieleza kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu imejipanga kuhakikisha inatekeleza majukumu na kazi zake kwa kasi zaidi ili kutimiza malengo ambayo wananchi wanayatarajia ikiwemo kutoa huduma bora na kutatua changamoto mbalimbali za wananchi, hivyo aliwataka watumishi wa Ofisi hiyo kufanya kazi kwa uzalendo na bidii.**

**“Tunakila sababu ya kujipanga sawasawa ili kuhakikisha yale tuliyofanikiwa tunayalinda na maeneo yale ambayo hatujafanya vizuri tunayafanyia kazi kwa kuboresha utendaji zaidi,” alisisitiza Waziri Mhagama.**


Inaendelea Uk. 4

Aidha, alieleza kuwa ujio wa Naibu Mawaziri wapya katika Ofisi hiyo ni ishara tosha kuwa sasa watumishi inabidi wawe katika hari mpya na nguvu mpya ili waendelee kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha na kutimiza malengo waliyokusudia.

Sambamba na hayo, Waziri Mhagama aliwahiza watumishi wa Ofisi hiyo kushirikiana pamoja na viongozi na kwa pamoja wajenge tabia ya kukumbushana uwajibikaji wa viwango wa hali ya juu na kutambua miiko ya utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa sheria za utumishi wa Umma.

Kwa upande wake, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira) Mhe. Patrobas Katambi amesema kuwa katika muhula huu wa pili anaimani kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu itaenda kutekeleza majukumu yake vizuri huku akiongezea kuwa ofisi hiyo itaendelea kushirikiana na Wizara nyingine mbalimbali katika kufanikisha gurudumu la maendeleo ya Taifa.

Naye, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Wenye Ulemavu) Mhe. Ummy Nderiananga amesema kuwa atahakikisha watumishi wa ofisi hiyo kwa pamoja wanashirikiana katika kushughulikia masuala mbalimbali ikiwemo yanayohusu wenye ulemavu ili kufanikisha malengo waliyokusudia kwa pamoja.



# HABARI KATIKA PICHA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akimuapisha Patrobas Paschal Katambi kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu) katika hafla iliyofanyika katika viwanja vya Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma tarehe 09 Desemba 2020.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akimuapisha Ummy Hamisi Nderinanga kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (wenye Ulemavu) katika hafla iliyofanyika katika viwanja vya Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma tarehe 09 Desemba 2020.

# WAZIRI MHAGAMA: "Wastaafu Walipwe Mafao kwa Wakati Kupunguza Malalamiko"




Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Jenista Mhagama ameitaka mifuko ya Hifadhi ya jamii kulipa mafao ya wanachama wao kwa wakati ili kuepuka malalamiko yasiyo ya lazima.

Ametoa kauli hiyo Desemba 18, 2020 alipokuwa akifunga semina ya siku tatu iliyolenga kuwajengea uwezo wajumbe wa Shirikisho la Mashirika ya Hifadhi ya Jamii (TSSA) na kuhudhuriwa na Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi mbalimbali wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Wakurugenzi Wakuu wa Mifuko hiyo.

Waziri alieleza, upo umuhimu wa kila mfuko kuona tija ya kulipa wanachama wao kwa wakati ili kuondokana na usumbufu unaoweza kujitokeza kwa wale wenye sifa za kulipwa na kusaidia wanachama hao kukidhi mahitaji yao kwa wakati mwafaka.

"Ni lazima kuhakikisha kuwa wanachama wanalipwa mafao yanayoendana na wakati ili kuwawezesha kukidhi matarajio yao bila kusahau wana mchango mkubwa katika mifuko yetu". alieleza waziri

Alifafanua kuwa, amekuwa akipokea malalamiko mengi kwa wastaafu kuhusu ucheleweshwaji wa mafao yao, hivyo kuonesha viashiria vya udhaifu kiutendaji na kuzielekeza mamlaka husika kutatua changamoto hiyo kwa weledi na ufanisi wa hali ya juu.

Aliongezea kuwa, mifuko inawajibu mkubwa wa kuhakikisha Waajiri wanaandikishwa na wanalipa michango kwa wakati.Idadi ya Waajiri ambao hawalipi michango imeongezeka hususan makampuni ya Ulinzi.

"Mifuko ipunguze usumbufu usikuwa wa lazima kwa wanachama hasa baada ya kustaafu na kudai mafao, kwa mfano mwanachama anastaafu akiwa na miaka 60 anaanza kudaiwa nyaraka ambazo aliwasilisha wakati anasajiliwa, kama kuna mabadiliko ya taarifa zinatakiwa zifanyiwe kazi na maafisa matekelezo kabla mwanachama kustaafu,"alisisitiza Waziri Mhagama

Aidha alieleza kuwa Azma ya Serikali ni kuona Watanzania wote wenye uwezo wa kufanyakazi wana andikishwa katika Mifuko ya Pensheni maana takwimu zinaonyesha bado kuna idadi kubwa ya wafanyakazi katika Sekta rasmi na isiyo Rasmi ambao bado hawajaandikishwa.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Mashirika ya Hifadhi ya Jamii (TSSA) Bw.William Erio alipongeza jitihada za Waziri na kuahidi kutekeleza maagizo yake aliyoyatoa pamoja na kuhakikisha wanakuwa na mikakati thabiti ya kushiriki katika miradi ya kimkakati ya Serikali.

## MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WA SEMINA YA WAJUMBE WA SHIRIKISHO LA MASHIRIKA YA HIFADHI YA JAMII (TSSA)



Waziri Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Mhe. Jenista Mhagama akimkabidhi cheti cha ushiriki Mkurugenzi Mkuu wa NSSSF Bw. Hosea Kashimba.




Katibu Mkuu wa Shirikisho la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Nchini (TSSA) Bw. Meshack Bandawe, akizungumza kuhusu shirikisho la Mifuko hiyo wakati wa mkutano wao mara baada ya kuhitimisha mafunzo ya siku Tatu ya TSSA yaliyofanyikamkoani Mwanza.





# SERIKALI KWA KUSHIRIKIANA NA VYAMA VYA WAFANYAKAZI MADEREVA NA VYAMA VYA WAMILIKI WA VYOMBO VYA USAFIRISHAJI WAJIPANGA KUIMARISHA SEKTA YA USAFIRISHAJI NCHINI




Serikali kwa kushirikiana na Vyama vya Wafanyakazi Madereva na Vyama vya Wamiliki wa Vyombo vya Usafirishaji kwa pamoja wamejipanga kushirikiana katika kupata ufumbuzi wa kero na changamoto mbalimbali ambazo zinaikabili sekta hiyo ya usafirishaji nchini.

Hayo yamebainishwa Disemba 19, 2020 Jijini Dodoma wakati wa kikao kazi cha mashauriano baina ya Serikali, Vyama vya Wafanyakazi Madereva na Vyama vya Wamiliki wa Vyombo vya Usafirishaji kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano uliopo jengo la PSSSF.

Akizungumza wakati wa kikao kazi hicho Kamishna wa Kazi, Brig. Gen. Francis Mbindi alieleza kuwa sekta ya usafirishaji inatoa mchango muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi, hivyo serikali imekua ikuchukua hatua madhubuti ili kuimarisha sekta hiyo.

“Sekta ya usafirishaji ni moja ya nyenzo muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote duniani, na ni dhairi serikali katika kulitambua hilo imeendelea kuimarisha sekta hiyo na kutatua changamoto ambazo zimekuwa zikijitokeza katika sekta hiyo,” alieleza Brig. Gen. Mbindi

Alieleza kuwa, wakati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli alipokuwa akifungua Bunge la 12 tarehe 13 Novemba, 2020 aliahidi kuwa serikali itahakikisha wamiliki wa magari wanatoa mikataba ya ajira kwa madereva ili kuipa hadhi inayostahili kazi hiyo na kuchochea shughuli za huduma za usafirishaji.

“Ninyi kama wadau muhimu wa sekta hii mna mchango mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa ahadi hiyo, na tuliona ni vema tukutane na kushauriana na kuweka mikakati ya pamoja,” alisema Brig. Gen. Mbindi


Inaendelea Uk. 10

Alifafanua kuwa baadhi ya kero na changamoto zimeweza kupatiwa ufumbuzi ikiwemo kuundwa kwa vyama vya wafanyakazi madereva ambavyo vimekuwa na mchango mkubwa katika kuleta uhuru wa madereva kwenye utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa sheria za kazi. Pia maboresho yamefanyika katika mkataba wa ajira ya madereva sambamba na makubaliano kuhusu viwango vya posho za safari kwa madereva ndani na nje ya nchi.


"Katika kusimamia utekelezaji wa mkataba ulioboreshwa mara kadhaa tumekuwa tukishirikiana nanyi katika kufanya ukaguzi kwenye vituo vikuu vya mabasi na baadhi ya maeneo ya kazi na kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi ili waweze kuzingatia matakwa ya sheria," alisema

Aliongeza kuwa, pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali katika kusimamia utekelezaji wa sheria lakini bado kumekuwa na changamoto katika utekelezaji wa sheria za kazi huku akitolea mfano wa baadhi ya waajiri wamekuwa hawatoi mikataba ya ajira kwa madereva, kutowapa haki wafanyakazi haki ya kujiunga na vyama vya wafanyakazi na kutowasajili na kuwachangia madereva kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

Aidha Kamishna wa Kazi amewataka Wafanyakazi Madereva na Wamiliki wa Vyombo vya Usafirishaji kuzingatia matakwa ya sheria za kazi wanapotekeleza majukumu yao.

Naye, Mwakilishi kutoka Chama cha Wafanyakazi wa Malori Tanzania (CHAWAMATA) Bw. Greyson Wimile alieleza kuwa wamefarijika na namna ambavyo serikali hii inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli imekuwa ikitatua changamoto zinazowakabili wafanyakazi madereva ikiwa ni kipaumbele kwa madereva kutambua wanathaminiwa na kazi hiyo wanayoifanya.








HERI YA KRISMASI NA MWAKA MPYA 2021